# MTIHANI WA BUNGOMA JOINT CHALLENGE

## DARASA LA NANE MUHULA WA PILI – 2021

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

**KISWAHILI**

Muda: Saa 1Dakika 40

1. Tumia penseli ya kawaida.
2. Hakikisha umeandika kwenye karatasi ya majibu:-
   (i) JINA LAKO (ii) JINA LA SHULE YAKO
3. Kwa kila swali, onyesha jibu sahihi kwa kuchora kijistari kwenye mabano ya alama ambayo umeichagua kuwa ndilo jibu sahihi.

***Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa kujaza nafasi zilizoachwa wazi:***

Heshima ni jambo _ 1 _ kwa baadhi ya wana wa leo. Wengine _ 2 _ heshima hata pasi kujua kwani mila na tamaduni zetu zimezikwa katika _ 3 _. Waama, _ 4 _. Hapo jadi kushiriki ngono kabla ya ndoa _ 5 _ ni mwiko. Kama jamii _ 6 _ kushughulikia jambo hili _ 7 _ dharura. _ 8 _ na mabaya kadri tuwezavyo.

1. A. ngeni B. geni C. mgeni D. kigeni
2. A. huwakosea B. humkosa C. hukosa D. humkosea
3. A. lindi la mawzo B. kaburi la sahau C. kaburi la buriani D. shimo
4. A. mtaka vyote hukosa vyote B. mvumilivu hula mbivu C. heshima si utumwa D. mwacha mila ni mtumwa
5. A. ilikuwa B. lilikuwa C. ulikuwa D. kilikuwa
6. A. inanibidi B. inatubidi C. inabidi D. inatubidii
7. A. na B. pamoja na C. kwa D. kuwa
8. A. Tujiepushe B. Tujiepuke C. Tuyaepukane D. Tuuiepukane

Kilimo _ 9 _ uti wa mgongo wa _ 10 _ wetu. Nasi hatuna budi _ 11 _ kikamilifu. Visa vya hivi punde vya ugaidi ambao umekuwa _ 12 _ kwetu vimechangia pakubwa _ 13 _ nyanja nyingine za mapato _ 14 _ utalii. Sasa ni lazima tutumie mbinu _ 15 _ ili kuboresha zaraa.

9. A. ndicho B. ndio C. ndiyo D. ndilo
10. A. uchumi B. chumi C. mapato D. uchumiko
11. A. kuuegemea B. kuitegemea C. kukiegemea D. kuiegemea
12. A. changudoa B. dondandugu C. mdondoakupe D. uhondo
13. A. kufilisisha B. kufululiza C. kufilisika D. kufilisia
14. A. licha ya B. mbali na C. hususan D. seuze
15. A. mipya B. mpya C. vipya D. mapya

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi kulingana na maagizo uliyopewa.***

16. Ni orodha ipi yenye sauti ghuna ?
    A. d, t, sh B. dh, th, gh
    C. d, gh, v D. ng, s, z

17. Andika katika usemi taarifa.
    "Nitamsubiri hadi kesho asubuhi", alisema
    A. Alimua kumsubiri hadi kesho asubuhi
    B. Alisema atamsubiri hadi siku iliyofuata asubuhi
    C. Aliamua angesubiri siku ifuatayo asubuhi
    D. Alisema kuwa angemsubiri hadi siku ifuatayo asubuhi

18. Chagua neno lenye herufi za sauti mwambatano.
    A. Mkoba B. Kitabu
    C. Ndizi D. Chakula

19. Tambua kiwakilishi katika sentensi ifuatayo:
    Mtoto wangu ni mrefu wake ni mfupi.
    A. wangu B. mrefu
    C. ni D. wake

20. Jaza pengo kwa msemo ufaao.
    Bwana Mpole alihudhuria maombolezi hayo ili kuwapa jamaa na marafiki ___
    A. mkono wa tahania
    B. mkono wa tanzia

C. Mkono wa buriani
D. Mkono wa heri

21. Ni sentensi ipi inayoonyesha 'kwa' ya sababu ?
A. Kaidi aliadhibiwa kwa utundu wake.
B. Alipata alama tisini kwa mia
C. Mwalimu aliandika kwa chaki
D. Mwalimu alienda kwa nyanyake

22. Eleza matumizi ya kiambishi-'Ki'kwenye hii sentensi.
*Nilipoenda kwao alikuwa akisoma kitabu cha kiswahili.*
A. Kuonyesha masharti
B. Kuonyesha hali ya kutenda
C. Kuonyesha wakati
D. Kuonyesha ngeli

23. Chagua kivumishi kwenye hii sentensi.
Wanafunzi shuleni mwetu ni wachache walioufeli mtihani wa mwigo
A. walioufeli
B. mtihani
C. wachache
D. mwigo

24. Andika sentensi bila kirejeshi –amba-
A. Mtoto ambaye husoma kwa bidii hufanikiwa.
B. Mtoto ambaye asomaye kwa bidii hufanikiwa
C. Mtoto anayesoma kwa bidii hufanikiwa
D. Mtoto husomaye kwa bidii hufanikiwa

25. Onyesha kielezi katika sentensi hii. Jana tulienda kutembelea mbuga ya wanyama ya Tsavo.
A. Jana
B. Kutembelea
C. Mbuga ya wanyama
D. Tulienda

26. Maelezo aligawa robo ya muwa sawasawa kwa wanawe wawili. Kila mmoja alipata __
A. nusu
B. robo mbili
C. sudusi
D. thumuni

27. Chagua sentensi iliyo sahihi.
A. Nilimokuwa palikuwa na giza
B. Niliokuwa mlikuwa na giza
C. Nilikokuwa mlikuwa na giza
D. Nilipokuwa kulikuwa na giza

28. Chagua umoja wa :
Wametuletea nyuzi tulizohitaji.
A. Ametuletea uzi niliouhitaji
B. Ameniletea nyuzi tulizohitaji
C. Ametuletea nyuzi tulizohitaji
D. Ameniletea uzi niliouhitaji

29. Ukitaka kujua uzito wa bidhaa zako utazipima kwa __
A. dira
B. nira
C. mizani
D. utepe

30. Ni mpangilio upi wa sentensi ulio sawa zaidi ?
A. Juma alihitimu, akajitahidi masomoni, akaajiriwa na akahojiwa.
B. Juma alijitahidi masomoni, akahitimu, akahojiwa na akaajiriwa
C. Juma aliajiriwa , akajitahidi masomoni, akahitimu na akahojiwa
D. Juma alihojiwa, akahitimu, akaajiriwa na akajitahidi masomoni

***<u>Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 31 – 40.</u>***

Ni jambo lisilopingika kuwa elimu ni ufunguo wa maisha. Aidha, ni nguzo imara ya kuegemea maishani. Hata hivyo, yafaa ifahamika kuwa elimu itamfaidi mumiliki wayo yule ambaye ataitumia kwa ufasaha. La muhimu zaidi, yule ambaye ataitumia kwa nidhamu, hekima na heshima hatajiuma kidole maishani.

Haijalishi iwapo mahuluku ameyasoma matopa ya vitabu. Haijalishi amefika kiwango kipi au anazo shahada zipi ? Iwapo hana adabu, heshima na uwajibikaji, elimu yake haijakamilika. Elimu hiyo si chochote si lolote. Elimu yake itakuwa kama pambo la wala si libasi. Pambo haliwezi kusitiri mtu. Hiyo ni kazi ya nguo.

Ni fedheha na izara kuwaona baadhi ya insi wakijitanua kifua kuwa wameelimika ilhali wanao fuska. Heshima kwao ni mwiko. Adabu na heshima ni maneno mageni. Mwalimu wangu wa zamani alinieleza kuwa kumiliki elimu ya aina hiyo ni sawa na kufunga tai huku ukiwa uchi wa mnyama.

Wanafunzi hawana budi kukakakawana na kupirikana masomoni. Wanapaswa kufahamu kuwa ufanisi hupatikana tu kupitia idili za magegenu wagugunavyo gogo. Aidha, wawe na msimamo imara na thabiti. Wasiwe bendera kufuata upepo. Wahenga husema kuwa nzi mmoja huoza ng'ombe.

Vijana ni faradhi wajitenge ,na wanaokaanga mbuyu na kuwaachia wenye meno kutafuna. Uzembe wauzike katika mava ya maghafala. Tangu hii kupakata mkoyo kukaleta fanaka? Vijana wafahamu kuwa ajizi ni nyumba ya njaa. Vilevile wajitanibu na vitatange wanaowatosa wengine demani. Wanaposhikwa sikio waweze kusikia na kushika mabange ya nasaha katika koleo za ubongo wao.

Ni jambo aula mtu kuonyesha elimu yake kwa vitendo. Vitendo vya yeyote aliye na elimu vinafaa viwe na mwelekeo na vya kutamanika. Vionyeshe ustaarabu bali si ushenzi isitoshe, ifahamike kuwa elimu si vitabu tu la hasha ! Ipo elimu dunia. Sharti elimu yetu ituwezeshe kutafakari ya dunia.

31. Kwa mujibu wa aya ya kwanza __
    A. Elimu humfaidi yeyote pasi na kujali nidhamu.
    B. Elimu huhitaji hekima ili kumsaidia mtu
    ₵. Elimu ni msingi madhubuti maishani
    D. Elimu haina uhusiano na maisha
32. Ili elimu itufaidi, hatuna budi kufanya nini ?
    A. Kuitumia kwa ufasaha na ujuvi
    Ƀ. Kusoma hadi kiwango cha juu
    C. Kudunisha nidhamu, hekima na heshima
    D. Kuitumia kwa nidhamu, heshima na akili

33. Maneno haijalishi iwapo mahuluku amesoma matopa ya vitabu yana maana.
    A. Mtu hutambulika kulingana na vitabu alivyosoma.
    Ƀ. Matopa ya vitabu yaliyosomwa huenda sambamba na maisha mazuri.
    C. Wenye adabu na heshima huwa hawajasoma matopa ya vitabu
    D. Adabu na uwajibikaji ndio msingi wa maisha wala si idadi ya vitabu vilivyosomwa.

34. Elimu bila adabu na uwajibikaji inamithilishwa na nini ?
    A. Nguo inayositiri mtu
    B. Kitu chochote chenye thamani
    C. Pambo lisiloficha uchi wa mja
    Đ. Vazi lisilo na thamani yoyote
35. Kwa mujibu wa habari ni jambo lipi la aibu ?
    A. Kuwaona wasomi waliojiingiza katika maovu hasa uasherati.
    Ƀ. Wakifunga tai huku wakiwa uchi wa mnyama.
    C. Waliosoma kuwadunisha na kuwadhalilisha wengine
    D. Wasomi kunyenyekea ,na kudumisha adabu a heshima
36. Neno mwiko lina maana gani ?
    Ⱥ. Jambo lisilofahamika vyema
    B. Jambo au kitu anachozuiwa mtu kufanya katika jamii
    C. Jambo linalokubalika katika jamii
    D. Jambo linalofanywa kwa mazoea na jamii

37. Mwanafunzi asiye na msimamo thabiti ni __
    A. Yule anayejiamulia mambo
    Ƀ. Yule anayezembea masomoni
    C. Yule anayefuata rubaa
    D. Yule anayejikakamua katika elimu
38. Ni nani anayenufaika kutokana na elimu ?
    A. Aliye na elimu ya juu
    B. Anayepata kazi baada ya elimu
    C. Anaye[illegible]a damu shuleni
    Đ. Anayeandamanisha elimu na mienendo ifaayo
39. Vijana wanashauriwa kufanya haya yote isipokuwa __
    A. kufanya ajizi masomoni
    Ƀ. Kujifunga masomba shuleni
    C. kutotetereka shuleni
    D. kujitenga na wanafunzi waovu
40. Kichwa mwafaka cha habari uliyoisoma ni kipi ?
    A. Elimu vitabuni
    B. Elimu mwafaka
    C. Elimu ya dezo
    Đ. Elimu dunia

***<u>Soma taarifa kisha ujibu maswali 41 – 50.</u>***

Katika mji wa Tushauriane paliishi bwanyenye mmoja aliyekuwa mkwasi tajika. Watu wengi walimpenda sana kwani alikuwa tajiri wa mali na moyo. Alimiliki mashangangi na jumba la kifahari. Kitendeni mwake kila siku mlishiba watu ili <u>awasabalie</u>. Kuna waliopewa riziki na wengine wakapewa vibarua. Yake alikuwa miongoni mwa walioajiriwa na bwanyenye huyo.

Yahe alikuwa maskini aliyedaiwa kope si zake. Alikuwa mkazi wa mji huo. Baada ya kupata kazi alipelekwa kiwandani ili awe akijizumbulia riziki yake pamoja na aila yake. Kila uchao alipiga milundi kwani hakumudu kupata nauli. Ungemwona njiani ungedhani <u>alichonekwa mizizi</u>. Njiani alijizungumzia, kichwa chake kikawa kizito kwa adha zilizomtinga.

Siku moja Yahe alijihimu kama ilivyokuwa ada yake. Aliamini ya wahenga kuwa ajizi ni nyumba ya njaa. Staftahi ilikuwa nadra na Fakizi kama shilingi ya siku za mwambo. Maswali mengi yalimzonga akilini na kumzunguka kama pia. Uhawinde na masaibu yalimfanya alengwelengwe na machozi.

Mwenyewe hakufahamu vipi watu wengine kama mwajiri wake walivyokuwa wakwasi wa kunuka pesa huku wengine kama yeye wakiishi maisha ya nunda mla watu.

Alipofika kazini, alikuwa amechelewa kwa saa moja. Kinyume na hapo awali alimkuta bwanyenye huyo mahali pake pa kazi. Alikuwa amepandwa na hasira za mkizi. Alishindwa vipi watoto wake aliowalea katika maisha ya fawaishi hawakuwahi kuchelewa ilhali Yahe angechelewa kwa saa moja. Jambo hili lilimfanya amkaripie Yahe huku akijisemea kimoyomoyo, "Mimi nilimtilia upondo aliponililia hali yake, kwani mja hutaka nini zaidi ?"

Yahe aliomba radhi kwa unyenyekevu mwingi. Hofu yake ilikuwa iwapo angejibizana na mwajiri wake huenda angepigwa kalamu, nayo mambo yamwendee zigizaga. Kulingana na yeye kamba yake ya matumaini ingekatika mara moja. Alishindwa kuelewa vipi tajiri wake angemzomea ilhali ilikuwa mara yake ya kwanza kuchelewa.

Maskini Yahe alihofia kutolipwa ujira wa siku hiyo kwani hilo lingetokea, watoto wake wangelalia mate. Ulipofika wakati wa adhuhuri Yahe hakuwa akihisi vyema. Aliporejea kazini aliendа miayo alasiri yote. Alijikusuru huku kazi ya kuvunja mgongo ikimtafuna kwelikweli.

Baadaye alimwendea bwanyenye aliyemwajiri ili apewe ujira wa siku hiyo. Ilikuwa vigumu kukubaliana na mwajiri wake lakini wakenya walisema kuwa ushikwapo shikamana. Alianza safari ya kurudi nyumbani huku mawazo yakigongana taamulini mwake mithili ya nyundo ya mhunzi kwenye fuawe.

41. Ni jambo lipi linaloonyesha kuwa bwanyenye alikuwa mkwasi wa mali na moyo ?
    A. Kuwa maskini mahitaji ya kimsingi
    B. Kuwa na mashangangi na kuwala muawana makabwela.
    C. Kuwa na mashangangi wa jumba la kumezewa mate.
    D. Waja wengine kufika kwake ili wanufaike.

42. Ni nini maana ya neno <u>awasabalie</u> kama lilivyotumika katika habari ?
    A. Awakopeshe pesa za kujikimu
    B. Awaajiri kazi ili wajiruzuku kibaba
    C. Awape mtaji wa kuasisi biashara
    D. Awasaidie bila kutarajia malipo

43. Kulingana na aya ya pili si kweli kusema kuwa _
    A. ilikuwa nadra Yahe kutembea hadi kazini
    B. Yahe aliwadai wengine haki yake
    C. Yahe alichapa kazi kiwandani
    D. Yahe alikuwa ameoa na kujaliwa wana

44. Ni nini maana ya <u>alichomekwa mizizi</u> ?
    A. Alifanyiwa uchawi
    B. Alitiliwa fitina
    C. Alichukuliwa na watu
    D. Alikuwa na mawazo mengi

45. Kisebele kilikuwa tukizi yaani __
    A. kilipatikana kwa wingi
    B. kilikuwa cha mazoea
    C. hakikupatikana kwa urahisi
    D. kilikuwa cha kuridhisha

46. Hatima ya aya ya tatu inadokeza kuwa __
    A. Yahe alitosheka na hali ilivyokuwa
    B. Yahe alikuwa na maswali mengi
    C. Yahe alishindwa kuelewa mbona watu wasiwe sawa kimaisha
    D. Yahe hakuelewa ni nini hufanya watu wengine maskini na wengine matajiri

47. Kwa mujibu wa habari maisha ya fawaishi ni yapi ?
    A. Maisha yenye uhitaji
    B. Maisha ya fahari na raha
    C. Maisha ya mjini
    D. Maisha ya raha na karaha

48. Maneno "Mimi nilimtilia upondo aliponililia hali yake, kwani mja hutaka nini zaidi ?" Yanaonyesha kuwa __
    A. Bwanyenye aliridhika na kujitolea kwa Yahe
    B. Bwanyenye alijua ni adhabu gani aliyofaa kwa hatia ya kuchelewa
    C. Tajiri alijua sababu ya Yahe kuchelewa
    D. Bwanyenye alitarajia Yahe kufika mapema ishara ya kushukuru kwa kazi.

49. Ni methali gani inayoafiki ujumbe huu : "Alishindwa kuelewa vipi tajiri wake angemzomea ilhali ilikuwa mara yake ya kwanza kuchelewa"
    A. Kosa moja haliachishi mke
    B. Baniani mbaya kiatu chake dawa
    C. Msafiri ni aliye bandarini
    D. Limatia limatia jongoo kukosa macho

50. ..... mawazo yakigongana taamulini mwake mithili ya nyundo ya mhunzi kwenye fuawe. Hii ni fani gani ya lugha ?
    A. Kinaya  B. Nahau
    C. Tashbihi  D. Istiara